117,525
679,336
354,500

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# SENSA YA WATU 1988

OFFICE OF CHIEF GOVERNMENT STATISTICIAN
LIBRARY
P.O. Box 2321
FAX: 223172
TEL: 223186
ZANZIBAR

*Kimetolewa na*

**OFISI KUU YA SENSA**
**IDARA YA TAKWIMU**
**Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango, Dar es Salaam**
**Machi, 1988**

Scanned with CamScanner

## SENSA YA WATU 1988

Mwaka huu tutakuwa na sensa ya watu ambayo itawahusu Watanzania wote, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Sensa ya watu ni kitu muhimu sana katika uhai na maendeleo ya Taifa lolote. Bila ya kuwa na takwimu muhimu za aina mbalimbali na zilizo sahihi na za kuaminika kazi ya Serikali ya kupanga na kuwahudumia wananchi itakuwa ngumu sana. Hivyo matokeo ya sensa ni nyenzo muhimu sana itakayoweza kutusaidia sisi sote katika upangaji mzuri wa mipango mbalimbali ya maendeleo.

Kutokana na umuhimu huu ufanisi wa shughuli za sensa ya 1988 ni wajibu wa kila mmoja wetu katika kila ngazi ya uongozi. Kila mmoja popote alipo awajibike ipasavyo.

Kwa upande wa wananchi ningependa kusema kuwa madhumuni makubwa ya shughuli hii ni WATU. Matokeo mazuri ya kazi hii ndiyo yatakayoiwezesha Serikali kuweza kuwahudumia wananchi vizuri baada ya kuelewa idadi yao, wapi walipo, wanavyoishi, matatizo yao na mahitaji yao.

Kwa ajili hiyo ninaomba msaada na ushirikiano wa kila mmoja wenu ili kufanikisha sensa ya mwaka huu. Wakati utakapowadia wa kuhesabu watu, nyote mjitokeze kuhesabiwa na kutoa majibu yaliyo sahihi.

Nawatakia wote kila la heri na ufanisi mzuri wa kazi hii.

JOSEPH S. WARIOBA,
*Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais,*
*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Dodoma,
20 Februari, 1988.

Scanned with CamScanner

## Yaliyomo


*Ukurasa*

| | |
|---|---|
| Utangulizi | 1 |
| Kwa nini Sensa? | 2 |
| Nini madhumuni ya Sensa? | 3 |
| Kujua idadi inasaidia vipi? | 3 |
| Maandalizi muhimu ya Sensa | 4 |
| Kutenga maeneo ya Kuhesabu Watu | 4 |
| Orodha ya Mabalozi na Kaya zake | 5 |
| Uteuzi wa Maofisa wa Sensa | 6 |
| Makamisaa wa Sensa | 6 |
| Kamati za Sensa | 7 |
| Wajibu wa Viongozi | 7 |
| Wajibu wa Wananchi | 8 |
| Maswali ya Sensa | 8 |
| Maswali ya Kujibiwa na wote | 8 |
| Maswali ya ziada ya fomu ndefu | 9 |
| Muhimu | 9 |
| Maswali yote yameidhinishwa | 10 |
| Majibu ya Sensa ni Siri | 10 |
| Maeneo Maalum ya Kuhesabu Watu | 10 |
| Wawindaji, Wavuvi, n.k. | 10 |
| Wasafiri | 11 |
| Mabalozi na Familia zao hapa Nchini | 11 |
| Watanzania Walio Nje | 12 |
| Siku ya Sensa | 12 |
| Tamko la Serikali | 12 |
| Matokeo ya Sensa | 12 |
| Mwisho | 13 |




Scanned with CamScanner

**Utangulizi:**

1. Mwezi Agosti mwaka huu itafanyika sensa ya kuhesabu watu wote Tanzania. Sensa hii itakuwa ni ya tatu kufanyika tokea nchi yetu kupata Uhuru. Kabla ya Uhuru sensa kama hizi zilifanyika mara sita.

2. Sensa hizo zilifanyika mwaka 1913, 1921, 1928, 1931, 1948 na 1957/58. Baada ya Uhuru sensa zilifanyika mwaka 1967, 1978. Sasa tunajiandaa kwa sensa ya Agosti, 1988.

3. Katika jedwali lifuatalo tunatoa muhtasari wa sensa zote zilizowahi kufanyika hapa nchini:—

| Mwaka | Idadi ya Watu | | |
|---|---|---|---|
| | Tanzania Bara | Tanzania Zanzibar | Jumla |
| 1913 | 4,115,777 | — | 4,115,777 |
| 1921 | 4,124,328 | 216,797 | 4,341,125 |
| 1931 | 5,063,660 | 235,428 | 5,299,088 |
| 1948 | 7,480,429 | 264,162 | 7,744,591 |
| 1957 | 8,788,466 | — | 8,788,466 |
| 1958 | — | 299,111 | 299,111 |
| 1967 | 11,958,654 | 354,815 | 12,313,469 |
| 1978 | 17,036,499 | 476,111 | 17,512,610 |

*Chanzo:* Ofisi ya Sensa, Idara ya Takwimu.

1988 22,455,193 640,685 23,095,878

2002 33,584,607 984,625 34,569,232

4. Tokea sensa ya 1978 mahesabu ya kitaalam yamekuwa yakionyesha kuwa ongezeko la Watanzania limekuwa likiongezeka kwa kiasi cha zaidi ya asilimia 3·2 kila mwaka. Kutokana na mahesabu hayo ya kitaalam inakisiwa kuwa idadi ya Watanzania wote hivi sasa (1988) ni milioni 23,997,000.

5. Lakini pamoja na makisio hayo bado haitoshi kuichukulia kuwa ndio idadi halisi ya watu wetu wote. Ili kuwa na uhakika wa idadi kamili ya watu wote ni mpaka wahesabiwe na hii ndio sababu ya sensa na umuhimu wake ili kupata hesabu ya uhakika juu ya idadi ya watu ambayo itakubalika kuwa ni sahihi na sio ya kubuni au kukadiria.



Scanned with CamScanner

6. Kwa makisio ya wataalam jedwali linaonyesha picha ya ongezeko la vatu kwa kila mkoa tokea sensa ya 1967.

| Mkoa | Idadi 1967 | Idadi 1978 | Makisio 1988 | Ongezeko kwa mwaka 1967/78 |
|---|---|---|---|---|
| Arusha .............. | 610,474 | 926,223 | 1,321,000 | 3.8 |
| Dar es Salaam ... | 356,286 | 843,090 | 1,723,000 | 7.8 |
| Dodoma ........... | 709,380 | 972,005 | 1,274,000 | 2.9 |
| Iringa .............. | 689,905 | 925,044 | 1,193,000 | 2.7 |
| Kagera ............. | 658,712 | 1,009,767 | 1,451,000 | 3.9 |
| Kigoma ............ | 473,443 | 648,941 | 851,000 | 2.9 |
| Kilimanjaro ....... | 652,722 | 902,437 | 1,193,000 | 2.9 |
| Lindi ................ | 419,853 | 527,624 | 645,000 | 2.1 |
| Mara ................ | 544,125 | 723,827 | 932,000 | 2.6 |
| Mbeya .............. | 753,765 | 1,079,864 | 1,469,000 | 3.3 |
| Morogoro ........ | 682,700 | 939,264 | 1,237,000 | 2.9 |
| Mtwara ............. | 621,293 | 771,818 | 934,000 | 2.0 |
| Mwanza ........... | 1,055,883 | 1,443,379 | 1,889,000 | 2.8 |
| Pwani ............... | 428,041 | 516,586 | 611,000 | 1.7 |
| Rukwa .............. | 276,091 | 451,897 | 684,000 | 4.5 |
| Ruvuma ........... | 395,447 | 561,575 | 758,000 | 3.2 |
| Shinyanga ......... | 899,468 | 1,323,535 | 1,839,000 | 3.5 |
| Singida ............ | 457,938 | 613,949 | 791,000 | 2.7 |
| Tabora ............. | 502,068 | 817,907 | 1,236,000 | 4.4 |
| Tanga ............... | 771,060 | 1,037,767 | 1,340,000 | 2.7 |
| Jumla Bara ... | 11,958,654 | 17,036,499 | 23,372,000 | 3.2 |
| Unguja ... | 190,494 | 270,807 | — | 3.2 |
| Pemba ... | 164,321 | 205,304 | — | 2.1 |
| Jumla Zanzibar. | 354,815 | 476,111 | 625,000 | 2.7 |
| Jumla Tanzania. | 12,313,469 | 17,512,610 | 23,997,000 | 3.2 |

*Chanzo:* Ofisi ya Sensa, Idara ya Takwimu.

## Kwa nini Sensa?

7. Jambo la kwanza ni muhimu ifahamike kuwa nchi zote ulimwenguni, zilizoendelea na zinazoendelea; maskini au tajiri; za Ulaya, Asia na hata Afrika zimejiwekea utaratibu wa kufanya sensa ya watu kwa misingi ya taaluma ya takwimu za nchi.

8. Kwa nchi zilizo nyingi, Tanzania ikiwa ni mojawapo, utaratibu unaofuatwa ni wa kufanya sensa kila baada ya miaka kumi, na hii ndio sababu tunaandaa sensa miaka kumi tokea sensa ya mwisho 1978.



Scanned with CamScanner

**Nini Madhumuni ya Sensa?**

9. Siasa ya Tanzania inayoongozwa na Azimio la Arusha na misingi ya Ujamaa na Kujitegemea na hivi karibuni Programu ya Chama cha Mapinduzi imeweka wazi kabisa kuwa shabaha ya siasa yetu au shabaha kubwa ya maendeleo yetu ni WATU.

10. Kwa misingi hii madhumuni makubwa ya kuandaa na kufanya sensa ni kupata takwimu zitakazotumika katika kupima kiwango cha maendeleo kilichofikiwa na kuandaa miongozo itakayotumika katika kutayarisha mipango ya maendeleo.

11. Kwa mantiki hiyo, basi, ni wazi kwamba ili mipango iweze kuandaliwa vizuri, tunahitaji kufahamu idadi ya watu, mahali walipo, mgawanyo wao kwa umri na idadi ya wanaume na wanawake, kazi wanazozifanya, kiwango chao cha elimu na ishara au dalili za ongezeko la watu hasa kuhusiana na idadi ya watoto wanaozaliwa na idadi ya watu wanaokufa. Takwimu kama hizi ndizo zinazosaidia sana katika kuandaa mipango ya maendeleo ya watu wetu.

**Kujua idadi inasaidia vipi?**

12. Baada ya Serikali kuelewa idadi ya watu katika nchi nzima kwa mkoa, wilaya, kata, na kwa kila kijiji, inakuwa rahisi sana kufikiria mipango ya maendeleo, huduma za kijamii kama vile maji, afya, elimu n.k. huduma za kiuchumi kama vile barabara, maghala, majosho, pembejeo za kilimo, n.k.

13. Mifano ifuatayo itasaidia kuelewa jinsi idadi ya watu inavyoweza kusaidia katika masuala mbalimbali ya maendeleo.

| Huduma | Idadi ya watu wanaotakiwa kuhudumiwa |
|---|---|
| 1. Huduma ya Zahanati Kijijini | 6,000—10,000. |
| 2. Huduma ya Kituo cha Afya | 50,000. |
| 3. Huduma ya Hospitali ya Wilaya | Kitanda kimoja kwa watu 1,000 kwa mwaka. |
| 4. Huduma ya Hospitali ya Mkoa | Kitanda kimoja kwa watu 1,000 kwa mwaka. |
| 5. Huduma ya Hospitali ya Rufaa | Kitanda kimoja kwa watu 1,000 kwa mwaka. |
| 6. Huduma ya Maji Vijijini | Lita 30 za maji kila siku kwa kila mwananchi. |
| 7. Huduma ya maji ya visima vifupi Vijijini | Siyo zaidi ya watu 250 kwa kila kisima. |
| 8. Kupata hadhi ya Mji Mdogo | Siyo chini ya watu 9,000. |
| 9. Kupata hadhi ya Mji | Siyo chini ya watu 30,000. |
| 10. Kupewa hadhi ya Manispaa | Siyo chini ya watu 80,000. |
| 11. Kupewa hadhi ya Jiji | Siyo chini ya watu 600,000. |
| 12. Kupata hadhi ya Kijiji | Siyo chini ya kaya 250. |



Scanned with CamScanner

14. Hii ni mifano michache tu ambayo inaonyesha jinsi idadi ya watu inavyoweza kusaidia Serikali na vyombo vingine vya Taifa katika kutoa maamuzi muhimu ya maendeleo. Kukosekana kwa hesabu ya watu na iliyo sahihi huweza kusababisha kushindwa kutoa maamuzi hayo haraka.

15. Kutokana na mifano hii tunaona kuwa iwapo kijiji fulani kina idadi ya kaya 92 tu, haiwezekani kwa kijiji hicho kupatiwa hadhi ya kuandikishwa kama kijiji wakati inajulikana kwamba idadi ya kaya zinazotakiwa kupata hadhi ya kijiji ni wastani wa kaya 250.

## Maandalizi Muhimu ya Sensa

16. Kama ilivyoelezwa hapo awali sensa hufanyika kila baada ya miaka kumi. Hivyo, sensa ya watu ni miongoni mwa miradi mikubwa ya ki-Taifa. Kwa ajili hiyo maandalizi yake huwa makubwa ili kuweza kufanikiwa katika lengo linalokusudiwa. Yafuatayo ni baadhi ya maandalizi muhimu ya sensa.

## Kutenga Maeneo ya Kuhesabu Watu

17. Ili kurahisisha kazi ya kuhesabu watu, nchi nzima inatengwa katika maeneo madogomadogo yatakayojulikana kama maeneo ya kuhesabu watu. Maeneo yote yatakayotengwa pia italazimu kuchorewa ramani zake kuonyesha mahali eneo lilipo na pia mipaka ya eneo hilo. Ramani hizo pia ndizo zitakazotumika wakati wa sensa kumwongoza kila mhesabuji katika eneo lake.

18. Katika kutenga maeneo hayo hakuna sehemu inayoachwa bila kutengwa hata kama ni misitu, bahari, mito, maziwa, milima, pori, mbuga za wanyama, n.k. Maeneo yote haya itabidi kutengwa na kujulikana.

19. Umuhimu wa kutenga maeneo haya ni kuhakikisha kuwa watu wote wanahesabiwa na mtu hahesabiwi mara mbili.

20. Kazi hii ya kutenga maeneo inafanyika katika mikoa yote hivi sasa na inatazamiwa iwe imekamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Machi, 1988.

21. Kulingana na taratibu za sensa ya mwaka huu kila eneo moja la sensa lililoko vijijini linatakiwa liwe na wastani wa watu 800 na katika maeneo ya mijini ambako kuna msongamano mkubwa wa nyumba na watu, kila eneo moja litatakiwa kuwa na wastani wa watu 400.

22. Chini tunatoa jedwali linaloonyesha idadi ya maeneo yanayotarajiwa kupatikana kwa kila mkoa kulingana na makisio ya watu.



Scanned with CamScanner

| Mkoa | Idadi ya Watu 1987 | Idadi ya Maeneo |
|---|---|---|
| Arusha | 1,274,000 | 1,787 |
| Dar es Salaam | 1,605,000 | 3,780 |
| Dodoma | 1,239,000 | 1,775 |
| Iringa | 1,167,000 | 1,723 |
| Kagera | 1,397,000 | 1,923 |
| Kigoma | 828,000 | 1,212 |
| Kilimanjaro | 1,159,000 | 1,529 |
| Lindi | 631,000 | 954 |
| Mara | 908,000 | 1,298 |
| Mbeya | 1,421,000 | 2,173 |
| Morogoro | 1,202,000 | 1,946 |
| Mtwara | 916,000 | 1,418 |
| Mwanza | 1,836,000 | 2,769 |
| Pwani | 600,000 | 850 |
| Rukwa | 656,000 | 1,029 |
| Ruvuma | 735,000 | 1,148 |
| Shinyanga | 1,779,000 | 2,453 |
| Singida | 770,000 | 1,208 |
| Tabora | 1,185,000 | 1,913 |
| Tanga | 1,305,000 | 1,919 |
| Jumla Bara ... | 22,611,000 | 34,807 |
| Jumla Zanzibar ... | 606,000 | 1,550 |
| Jumla Tanzania ... | 23,217,000 | 36,357 |

*Chanzo:* Ofisi ya Sensa, Idara ya Takwimu.

**Orodha ya Mabalozi na Kaya zake**

23. Ili kuhakikisha kuwa unakuwepo ufanisi mzuri katika kazi ya kutenga maeneo ya kuhesabu watu inabidi kwanza iwe imepatikana orodha kamili ya mabalozi na wakuu wote wa kaya nchini, kwa majina.

24. Orodha hiyo pia itatakiwa kuonyesha idadi ya watu wote wanaoishi katika kaya hizo.

25. Umuhimu wa orodha hii ni kuwa wakati utakapowadia wa kuhesabu watu, wahesabuji wote watakuwa na orodha ya mabalozi na majina ya wakuu wa kaya walio katika eneo lake. Hii itasaidia mhesabuji kuhakikisha kuwa watu wote katika eneo lake wanahesabiwa na baada ya kumaliza haingii katika eneo lingine.



Scanned with CamScanner

26. Kazi ya kupata orodha hii ni moja tu ya mbinu za kufanikisha shughuli nzima ya sensa, na wala isichukuliwe kuwa inaweza kuwa badala ya sensa halisi kwa vile wakati wa kuchukua orodha hiyo watu hawakutakiwa kujibu maswali yeyote ya sensa kama itakavyoonekana hapo baadaye.

27. Kutokana na umuhimu huu, iwapo kutakuwepo balozi yeyote ambaye ana hakika hajatembelewa na jina lake kuchukuliwa pamoja na majina ya wakuu wote wa kaya zake, tafadhali ajitahidi kuonana na Katibu wa Tawi kwa maeneo ya mijini au Mwenyekiti/Katibu wa kijiji ili kuhakikisha kuwa yeye na wakuu wa kaya zake wameorodheshwa.

28. Ili kufanikisha zoezi hili, viongozi wote wa mashina na pia wakuu wa kaya watoe kila aina ya msaada na ushirikiano kwa viongozi watakaowatembelea kwa kuwapatia orodha hizo.

## Uteuzi wa Maofisa wa Sensa

29. Kama inavyoeleweka, sensa inafanyika kote nchini Tanzania. Ili kupata ufanisi mzuri wa shughuli za sensa Maofisa wa Sensa wameteuliwa kwa kila mkoa na kila Wilaya. Majukumu yao muhimu ni kusimamia na kuhakikisha kuwa shughuli zote za sensa katika maeneo yao zinakwenda vizuri. Vilevile wao ndiyo kiungo muhimu cha shughuli za sensa kati ya mikoa na Ofisi Kuu ya Sensa.

## Makamisaa wa Sensa

30. Ili kufanikisha sensa inabidi kufanyika kazi kubwa ya kuelimisha na kuhamasisha Umma. Wananchi wanapoelimishwa juu ya umuhimu wa sensa na faida zake kwa Taifa ndivyo itakavyokuwa rahisi kupata msaada na ushirikiano wao.

31. Jukumu hili liko mikononi mwa Makamisaa wa Sensa (mmoja kwa upande wa Tanzania Bara na mwingine kwa upande wa Zanzibar). Wajibu wao mkubwa ni kuongoza maandalizi yote ya sensa kisiasa nchini na wanakuwa ndiyo kiungo muhimu wa Chama, Serikali, wataalam na wafanyakazi wote wanaojishughulisha na mradi huu wa sensa.

32. Lakini kama ilivyoelezwa, wajibu huu wa kuhamasisha Umma unawahusu pia viongozi wote wa Chama na Serikali katika kila ngazi ya uongozi. Ni hapo unapokuwepo ushirikiano na mshikamano mzuri wa viongozi wote ndipo kunaweza kuwepo na ufanisi mzuri wa shughuli za sensa.



Scanned with CamScanner

## Kamati za Sensa

33. Ili kufanikisha shughuli za sensa imebidi pia ziundwe kamati mbalimbali ambazo zina majukumu ya kuratibu mipango, utekelezaji na ufanisi wa kazi za sensa.

34. Katika ngazi ya Taifa zitakuwepo Kamati mbili: Moja ya Mawaziri ambayo Mwenyekiti wake ni Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais. Kazi ya kamati hii ni kutoa miongozo na maamuzi ya kisera katika utekelezaji wa mpango mzima wa sensa ya 1988.

35. Kamati ya pili ni ya Makatibu Wakuu ambayo Mwenyekiti wake ni Katibu Mkuu katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais. Kamati hii ya wataalam itakuwa ni ya utendaji zaidi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio, maamuzi na maagizo mbalimbali yaliyoamuliwa na kamati ya Mawaziri.

36. Kamati zingine ni za ngazi ya Mikoa na Wilaya ambazo Wenyeviti wake ni Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya.

37. Majukumu makubwa ya kamati hizi pia ni kufuatilia shughuli za sensa za siku hadi siku na kufuatilia matatizo yote yanayoweza kuathiri ufanisi wa sensa kwa kuyapatia ufumbuzi.

38. Matatizo hayo ni pamoja na ya usimamizi wa maandalizi yote ya sensa kwa ujumla, kupata orodha ya mabalozi na wakuu wote wa kaya, kutenga maeneo na kuchora ramani zake, maandalizi ya wale watakaohesabu watu, matatizo ya mipaka, usafiri, mafuta, usalama wa wahesabuji, n.k.

## Wajibu wa Viongozi

39. Viongozi wote wa Chama, Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Taasisi, Vyama vya Ushirika, Serikali za Mitaa na Vijiji wana jukumu la kuona kuwa sensa inafanikiwa. Ushirikiano wao na mshikamano mzuri wa hali ya juu wa viongozi katika ngazi zote utatakiwa ili kupata ufanisi wa zoezi hili.

40. Pia Viongozi wote watawajibika katika suala zima la kuandaa Umma kwa kuwaelimisha na kuwahamasisha kuhusu umuhimu wa sensa ili kupata msaada na ushirikiano wao wakati wa sensa. Kazi hii itafanyika kwa njia za vikao mbalimbali vya Chama na Serikali, katika semina, mikutano ya hadhara na pia kwa njia zinginezo za maandishi, vielelezo na pia mabango.

41. Mbinu zinginezo ni pamoja na kuwatumia wanafunzi mashuleni, vyuoni na katika majeshi kwa njia za nyimbo, kwaya, michezo ya kuigiza, ngonjera, ngoma za utamaduni, n.k. Vilevile bendi za dansi, taarab na vikundi vya aina mbalimbali za burudani ambazo zipo karibu katika kila mkoa.



Scanned with CamScanner

42. Viongozi wote wa dini na madhehebu mbalimbali nao wana jukumu la kusaidia katika kufanikisha sensa kwa kuwaelimisha waumini wao juu ya umuhimu wa sensa.

43. Msaada wa Viongozi wa mashina hapa ni muhimu sana kwa vile sensa itafanyika katika mashina yao. Kwa hiyo msaada na ushirikiano wao utahitajika kwa kuwatembeza wahesabuji katika maeneo yao, kuhakikisha usalama wao na pia kuhakikisha majibu yanayotolewa ni sahihi na ya kweli.

### Wajibu wa Wananchi

44. Kama ilivyoelezwa hapo awali sensa ni muhimu sana katika kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo. Hivyo, taarifa na takwimu zinazotafutwa ni vitu vinavyogusa maisha ya kila mtu anaeishi Tanzania.

45. Kwa ajili hiyo watu wote wanaombwa wakati wa sensa kuonyesha moyo wao wa ushirikiano kwanza kwa kujitokeza ili kuhesabiwa na pili kwa kutoa majibu sahihi. Ni kutokana na msaada na ushirikiano wa wananchi ndiyo malengo ya sensa yanaweza kupatikana na kufanikiwa.

46. Inasisitizwa kwamba sensa hii (1988) imeruhusiwa kwa mujibu wa sheria ya nchi. Habari zote zitakazotolewa zitakuwa za siri. Yeyote atakayevunja sheria hii ya kutunza siri, atachukuliwa hatua za kisheria.

### Maswali ya Sensa

47. Maswali ya sensa yatakayoulizwa yatakuwa katika mfumo wa aina mbili za fomu: fomu ya maswali machache na fomu ya maswali mengi.

48. Mahali ambapo fomu za maswali machache zitatumika kuhesabu watu fomu za maswali mengi hazitatumika na pale ambapo fomu za maswali mengi zitatumika fomu za maswali machache hazitatumika.

49. Katika sehemu kubwa ya nchi fomu ya maswali machache ndiyo itakayotumika kuhesabu watu.

50. Fomu ya maswali mengi itatumika katika maeneo machache sana katika kila mkoa na kila wilaya ambayo yatachaguliwa kwa kutumia utaalam wa hali ya juu.

### Maswali ya kujibiwa na wote

51. Lakini popote pale fomu hizi zitakapotumika maswali muhimu machache itabidi kujibiwa na watu wote. Ni vema kuelewa kuwa katika kuyajibu vizuri, maswali haya ndiyo yatakayowezesha kupata idadi ya watu wote hapa nchini kwa haraka iwezekanavyo.

52. Maswali haya yatataka kujua kwanza, jina la mkuu wa kaya, pili watu wote waliolala katika nyumba hiyo katika usiku wa sensa (27/28 Agosti, 1988) na tatu uhusiano wa watu hao na mkuu wa kaya.



Scanned with CamScanner

42. Viongozi wote wa dini na madhehebu mbalimbali nao wana jukumu la kusaidia katika kufanikisha sensa kwa kuwaelimisha waumini wao juu ya umuhimu wa sensa.

43. Msaada wa Viongozi wa mashina hapa ni muhimu sana kwa vile sensa itafanyika katika mashina yao. Kwa hiyo msaada na ushirikiano wao utahitajika kwa kuwatembeza wahesabuji katika maeneo yao, kuhakikisha usalama wao na pia kuhakikisha majibu yanayotolewa ni sahihi na ya kweli.

### Wajibu wa Wananchi

44. Kama ilivyoelezwa hapo awali sensa ni muhimu sana katika kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo. Hivyo, taarifa na takwimu zinazotafutwa ni vitu vinavyogusa maisha ya kila mtu anaeishi Tanzania.

45. Kwa ajili hiyo watu wote wanaombwa wakati wa sensa kuonyesha moyo wao wa ushirikiano kwanza kwa kujitokeza ili kuhesabiwa na pili kwa kutoa majibu sahihi. Ni kutokana na msaada na ushirikiano wa wananchi ndiyo malengo ya sensa yanaweza kupatikana na kufanikiwa.

46. Inasisitizwa kwamba sensa hii (1988) imeruhusiwa kwa mujibu wa sheria ya nchi. Habari zote zitakazotolewa zitakuwa za siri. Yeyote atakayevunja sheria hii ya kutunza siri, atachukuliwa hatua za kisheria.

### Maswali ya Sensa

47. Maswali ya sensa yatakayoulizwa yatakuwa katika mfumo wa aina mbili za fomu: fomu ya maswali machache na fomu ya maswali mengi.

48. Mahali ambapo fomu za maswali machache zitatumika kuhesabu watu fomu za maswali mengi hazitatumika na pale ambapo fomu za maswali mengi zitatumika fomu za maswali machache hazitatumika.

49. Katika sehemu kubwa ya nchi fomu ya maswali machache ndiyo itakayotumika kuhesabu watu.

50. Fomu ya maswali mengi itatumika katika maeneo machache sana katika kila mkoa na kila wilaya ambayo yatachaguliwa kwa kutumia utaalam wa hali ya juu.

### Maswali ya kujibiwa na wote

51. Lakini popote pale fomu hizi zitakapotumika maswali muhimu machache itabidi kujibiwa na watu wote. Ni vema kuelewa kuwa katika kuyajibu vizuri, maswali haya ndiyo yatakayowezesha kupata idadi ya watu wote hapa nchini kwa haraka iwezekanavyo.

52. Maswali haya yatataka kujua kwanza, jina la mkuu wa kaya, pili watu wote waliolala katika nyumba hiyo katika usiku wa sensa (27/28 Agosti, 1988) na tatu uhusiano wa watu hao na mkuu wa kaya.



Scanned with CamScanner

53. Uhusiano huo unaweza kuwa ni mke, mtoto, ndugu, baba, mama, kaka, dada, mjomba, wifi, shangazi, rafiki, mgeni, au jamaa tu.

54. Maswali mengine yatakayofuata yatataka kujua umri wa kila mmoja na uraia wake.

## Maswali ya ziada ya fomu ndefu

55. Kwa wale watakaokuwa na bahati ya kuulizwa maswali kutoka fomu ndefu watawajibika kujibu maswali ya ziada ambayo:—

(i) yatawahusu watu wote;
(ii) yatawahusu watu walio na umri wa miaka mitano na zaidi;
(iii) yatawahusu wanawake wote walio na umri wa miaka 12 na zaidi;
(iv) yatahusu vifo katika jamii na;
(v) yatahusu nyumba za kuishi na mazingara yake.

56. Maswali yanayohusiana na kifungu cha (ii) ni elimu na kazi: Kama unajua kusoma na kuandika Kiswahili; kama umesoma umefikia kiwango gani cha elimu, na unasoma darasa la ngapi iwapo kwa sasa ni mwanafunzi.

57. Maswali yanayohusiana na kifungu cha (iii) ni uzazi: Idadi ya watoto aliowahi kuzaa wakiwa hai. Katika hao wangapi mama anaishi nao wote, wangapi wanaishi mbali na mama: na wangapi wamefariki. Na pia idadi ya watoto aliozaa wakiwa hai kati ya Agosti mwaka jana na wakati anapojibu maswali haya.

58. Maswali yanayofuata ni kuhusu vifo vilivyotokea katika jamaa kwa ujumla katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kati ya Agosti 1987 na Agosti 1988: idadi yao, umri na jinsi (wakike au wakiume).

59. Vile vile yatakuwepo maswali yanayotaka kujua iwapo mama mzazi bado anaishi; hali ya ndoa; mahali pa kuzaliwa; masikani; na sensa ya mwaka 1978 ilimkuta wapi.

60. Maswali kuhusu nyumba yatataka kujua nyumba ni ya vyumba vingapi, kama inamilikiwa na Mkuu wa Kaya au ni ya kupanga, kama nyumba ina choo, maji au umeme?

## Muhimu

61. Kama ilivyoelezwa hapo awali maswali yote haya yana lengo la kukidhi mahitaji mbalimbali ambayo Taifa linahitaji kwa wakati wa hivi sasa na huko baadaye kwa ajili ya upangaji na utekelezaji mzuri wa mipango mbalimbali ya maendeleo.

62. Hivyo, mkuu wa kaya anaombwa sana ayaelewe na ayazingatie maswali yote haya ili aweze kuyajibu kwa ufasaha.



Scanned with CamScanner

63. Hapa ni vizuri pia kutoa jambo la tahadhari kuwa inawezekana katika usiku wa sensa, mgeni alilala nyumbani na kesho yake akawa ameondoka. Kwa utaratibu wa sensa mgeni huyo atatakiwa kuhesabiwa hapo alipolala na siyo huko atakakokutwa siku tano baadaye. Kwa ajili hiyo ni vizuri kwa mkuu wa kaya kuzingatia majibu ya maswali haya kabla ya kuagana na mgeni wake awe na majibu ya maswali yote haya ili aweze kuyajibu maswali ya sensa kwa niaba ya mgeni wake.

**Maswali yote yameidhinishwa**

64. Tunapenda kuwajulisha wananchi wote kuwa maswali yote ya sensa yamepitiwa na kuidhinishwa na Kamati Kuu ya Sensa ya Taifa chini ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais kama Mwenyekiti.

**Majibu ya Sensa ni Siri**

65. Ni muhimu kusisitiza tena kuwa taarifa zote zitakazotolewa wakati wa sensa ni siri kubwa kati ya mhesabuji na mjibu maswali. Wote watakaohusika katika sensa watakuwa wamekula kiapo cha uaminifu kuhifadhi siri kwa yote watakayokuwa wameyapata wakati wa sensa. Hivyo wananchi wote wanaombwa wasiogope au wasisite kutoa taarifa zozote watakazoulizwa kwa kuogopa kuwa siri itatoka nje.

**Maeneo Maalum ya Kuhesabu Watu**

66. Mbali na maeneo yaliyoelezwa juu ya kuhesabu watu ambapo watu watahesabiwa majumbani mwao, pia yapo maeneo ambayo ni tofauti, na yatakuwa na watu ambao, kwa mujibu wa taratibu za sensa itabidi na wao wahesabiwe.

67. Maeneo hayo ni mahospitalini, vyuo, mashule, kambi za wanajeshi, kambi za wakimbizi na nyumba za kulala wageni.

68. Wote watakaokuwa katika maeneo hayo katika usiku wa sensa watakuwa na mtu maalum wa kupitia maeneo hayo yote na kuwahesabu. Ombi kwa watu hawa ni kuwa iwapo asubuhi ya mkesha wa sensa wataondoka katika maeneo hayo, kwa mfano iwapo walikuwa wamelazwa hospitalini na kurejea majumbani mwao, wasikubali kuhesabiwa tena huko walikokwenda kwa vile hesabu yao itakuwa imechukuliwa pale walipolala. Vinginevyo itakuwa ni kuhesabiwa mara ya pili, na hii inaweza ikaleta dosari katika kupata mahesabu sahihi ya idadi ya watu.

**Wawindaji, Wavuvi, n.k.**

69. Katika jitihada za kuhakikisha kuwa kila mtu anahesabiwa na anahesabiwa mara moja tu, kuna makundi mbalimbali ya watu ambayo yatatakiwa yatoe ushirikiano mzuri katika kufanikisha kazi ya kuhesabu makundi hayo.



Scanned with CamScanner

70. Moja ya makundi hayo ni lile la wawindaji, wavuvi, wapakua asali, watafutaji madini, na pia baadhi ya wakulima ambao wana mashamba yaliyo mbali na majumbani mwao.

71. Itakuwa sio rahisi kwa wahesabuji kuelewa ni wapi walipo ili kuweza kufuatwa huko na kuhesabiwa. Kwa ajili hiyo watu hawa wanaombwa kuhakikisha kuwa siku ya sensa wanajitahidi kurudi majumbani mwao ili wapate kuhesabiwa. Vinginevyo itakuwa ni vigumu kwao kuhesabiwa na Taifa litakuwa limepata upungufu mkubwa sana kwa wao kutohesabiwa.

**Wasafiri**

72. Kundi lingine la watu ambao na wao itabidi kupata ushirikiano wao ni wasafiri. Ni wazi magari, ndege, treni, meli, n.k. zitakuwa zinasafiri na watakuwepo watu watakaosafiri katika vyombo hivyo. Pamoja na kwamba watu hao tungependa kuwaomba siku hiyo ya sensa wasisafiri, lakini haitawezekana kuzizuia safari zote kutokana na umuhimu wake.

73. Ili kundi hili la watu lipate kuhesabiwa, utaratibu umefanywa kwamba wahesabuji watakuwa katika vituo vyote vya usafiri, yaani vituo vya mabasi, stesheni za reli, viwanja vya ndege na bandari zote na kuhakikisha kuwa wasafiri wote wanahesabiwa kabla ya kuondoka usiku huo, au wanahesabiwa mara baada ya kuwasili katika vituo wanapoteremkia.

74. Wote watakaokuwa katika kundi hili wanaombwa washirikiane na wahesabuji katika kufanikisha kazi ya kuhesabu. Kama wataanza safari yao kabla ya usiku wa sensa na kuwasili kesho yake au baadaye, basi, wahakikishe wanahesabiwa katika vituo vya kuteremkia. Iwapo wamehesabiwa kabla ya kuondoka waepukane na kuhesabiwa mara ya pili huko watakakoishia. Na kama wataondoka baada ya kulala katika nyumba lakini kabla ya mwesabuji hajapita wasihesabiwe huko wanakoteremkia kwani wao watahesabiwa katika nyumba waliokuwa wamelala katika usiku huo wa sensa.

75. Kundi lingine ambalo hatuna budi kuligusia hapa ni la watu ambao hawana nyumba na au mahali maalum pa kuishi. Nao hao Serikali pia ina haja ya kupata idadi yao. Tungewaomba na wao wakati wa sensa kujitokeza popote pale na kuhesabiwa.

76. Nia ya Serikali ni kujua idadi ya watu wote, na wao kama Wazalendo na Watanzania ni budi hesabu yao ijulikane.

**Mabalozi na Familia zao hapa Nchini**

77. Kwa utaratibu wa sheria za kimataifa mabalozi wote pamoja na familia zao popote pale watakapokuwa hutambuliwa kama wapo kwenye nchi zao. Kwa ajili hiyo mabalozi wa nchi za kigeni waliopo Tanzania hawatahesabiwa siku ya sensa.



Scanned with CamScanner

78. Ila kama watakuwa na watumishi au wasaidizi wa aina yeyote watakaokuwa wamewaajiri kuwasaidia kazi, na hawana hadhi ya kibalozi, hao wote kwa mujibu wa sheria itabidi kuhesabiwa.

## Watanzania Walio Nje

79. Sensa itakayofanyika itawahusu watu wote watakaokuwa hapa nchini katika siku ya sensa, walio raia na wasio raia (ukiondoa wale wote wenye hadhi za ubalozi). Wote watakaokuwa nje ya mipaka ya nchi yetu siku hiyo ya sensa hawatahusika katika zoezi hili.

## Siku ya Sensa

80. "Siku ya Sensa" imepangwa kuwa ni usiku wa Jumamosi, tarehe 27 Agosti, kuamkia siku ya Jumapili, tarehe 28 Agosti, 1988. Kwa ajili hiyo, kulingana na taratibu za kisensa, kazi ya kuanza kuhesabu watu itaanzia asubuhi ya siku hiyo ya Jumapili na kazi itatakiwa kuendelea mpaka kuhakikisha kuwa kazi imemalizika na wote wamehesabiwa.

81. Siku hii ya sensa imepangwa kwa maana kuwa itakuwa imefikia kipindi kamili cha miaka 10 tokea sensa ya mwisho ya mwaka 1978, ambayo ilifanyika pia siku ya Jumapili, tarehe 27 Agosti.

## Tamko la Serikali

82. Ili sensa ya kuhesabu watu iweze kufanyika kisheria litatolewa tamko rasmi la Serikali la kuidhinisha sensa kufanyika. Kwa mujibu wa sheria, tamko rasmi la Serikali (Census Order) litatolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Gazeti la Serikali kama tangazo la Serikali.

## Matokeo ya Sensa

83. Kama itakavyokuwa imeonekana maswali ya sensa ni mengi na yanayohusu mambo mengi tofauti. Kwa ajili hiyo kuweza kuchambuliwa yote na kupata majibu yake katika kipindi kifupi siyo kazi rahisi. Ni wazi muda mrefu utahitajika ili kuweza kuyachambua yote kwa uangalifu mkubwa ili kuweza kupata majibu na matokeo sahihi.

84. Lakini lililo wazi na ukweli ni kuwa matokeo ya idadi ya watu wote ni kitu kinachotakiwa kipatikane haraka iwezekanavyo. Kwa ajili hiyo matokeo hayo tunategemea yatangazwe na Serikali mwishoni mwa mwezi Desemba, 1988.



Scanned with CamScanner

**Mwisho**

85. Kama ilivyokwishaelezwa katika makala haya, sensa ni kiungo muhimu sana kinachosaidia Serikali katika kufikia maamuzi, au kusaidia uandaaji mzuri wa mipango mingi ya maendeleo.

86. Kwa mantiki hiyo ni mategemeo yetu kuwa wananchi wote, raia na wageni watajitokeza kuhesabiwa na kutoa majibu sahihi kwa maswali yote ya sensa.

87. Kwa upande wa viongozi wa Chama, Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Vyama vya Ushirika, Vijiji na Madhehebu ya Dini, ni matarajio yetu kuwa wote watashiriki ipasavyo ili kufanikisha mpango huu.

INAWEZEKANA IWAPO KILA MMOJA ATATIMIZA WAJIBU WAKE



Scanned with CamScanner